

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI

21 MEI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 21 MEI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

##### **390. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO (BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini zoezi la kuhamia Dodoma litakamilika na Taasisi ngapi zimeshahamia Dodoma.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **391. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Wataalam wa X-Ray na Ultra Sound watapelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Chemba.

##### **392. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA (KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Zahanati katika kila Kijiji nchini ili kusogezza huduma za afya kwa Wananchi.

**393. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga uzio kwenye Shule zote za Bweni za Wasichana Wilayani Urambo.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**394. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, kuna Mbwa wangapi nchini.

**WIZARA YA MAJI:**

**395. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka gari RUWASA Wilaya ya Nyasa.

## **WIZARA YA UCHUKUZI:**

### **396. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ukarabati wa Reli ya Kati kwa kuwa miundombinu yake ni chakavu.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **397. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, upi ukomo wa kuweka alama za upana wa Barabara Vijijini na kuwataka Wananchi kubomoa nyumba kutumia Sheria ya Mwaka 1932 na 2007.

### **398. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya barabara katika Jiji la Mwanza.

**399. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, hadi sasa ni kilometra ngapi zimejengwa kwa kiwango cha lami Barabara ya Mbalizi-Mkwajuni.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**400. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPER KABATI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi ya Polisi ya Wilaya ya Kilolo.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**401. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha Vyuo vya Mafunzo katika Fani za Kilimo, Mifugo na Ufundu ili kuwawezesha Vijana kupata Elimu ya Ufundu.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **402. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua zao la Nazi katika Ukanda wa Pwani hususan Bagamoyo ili kuleta tija kwa wananchi.

## **WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **403. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, lini Serikali itaamua kuwekeza kwa nguvu katika Viwanja, Walimu na Mawakala wa michezo inayoonekana kuleta tija kwa Taifa letu.

### **404. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kwa nini Tamaduni za kigeni zimetawala sanaa zetu kuliko utamaduni wetu wakati BASATA ipo kuhimiza na kukuza utamaduni wetu.

#### **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA**  
**21 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***  
**KATIBU WA BUNGE**